

LEARNING BY EAR 2009

Economics – 8th episode

SUCCEEDING IN THE BUSINESS WORLD

Series: “THE STORY OF TWO YOUNG PEOPLE, WHOSE SUCCESS STEMS FROM THEIR POCKET MONEY”

Author: Frédéric GAKPARA

Editors: Yann Durand and Sandrine Blanchard

Translator: Anne Thomas

Kisuaheli : Eric Ponda

EIGHTH EPISODE: "Between two airports"

Characters: **Jane** (*20 years old, commercial director AOTT*)

Dad (*Jane's dad, 49 years old*)

Granma (*Jane's grandmother, 70 years old*)

Mrs Sika (*24 years old, Secretary at AOTT*)

Miss Mable (*22 years old, former schoolmate of Jane*)

Stewardess' voice for airport announcements, Scene2

Learning by Ear Soundtrack

Intro

NARRATOR: Hujambo msikilizaji na karibu kwa makala nyingine ya Learning By Ear “Noa Bongo Jenga maisha yako” kuhusu hadithi ya vijana Mapacha ambao wamepata ufanisi wa kicuhumi kupitia juhudi za kubania matumizi na kuanzisha biashara. Sasa ni miaka miwili tangu John na Jane wasafirishe shehena yao ya kwanza katika soko la Bara Ulaya. Na tangu wakati huo hawajarudi nyuma. Biashara imeendelea vizuri. Sasa mapacha hawa wametimu umri wa miaka 20. Wameweza kuawajiri zaidi ya wafanyi kazi 300 viwandani na ofisini. Kampuni yao ya "Appetizers of the Tropics" (AOTT) imepanua biashara zake na sasa imeanza kuuza matunda yaliyokaushwa na siagi. Pia mapacha hawa bado wanaendelea na msomo yao. Jane meneja wa kampuni hiyo anaendelea kuwahudumia wageni tunapoingia makala ya nane”

Scene 1, IN JANE'S OFFICE

JANE, GRANMA, MRS SIKA, MISS MABLE...

ATMO: *Air conditioning. Sounds of printer and photocopier. The intercom rings.*

- Jane:** Hallo, naam, hallo.... Bibi Sika? Bibi amefika? , Sawa waambie wanisubiri dakika chache.

2. **ATMO:** *We hear Jane's steps and her opening the door... The office echoes her voice... We hear the sound of a fax...*
3. **Jane:** Ohhh, Bibi! Nimekuahidi nitakupitia kabla ya kwenda uwanja wa ndege . Kwanini umejisumbua na safari yote hiyo?. Karibu ndani..! lazima umechoka!
4. **Granma:** Ohhh! Mjukuu wangu Jane una kazi nyingi, hata labda ungenikumbuka ukiwa uwanja wa Ndege.!
5. **ATMO:** *They go into the office.*
6. **Jane:** Hapana Bibi ! Hiyo ilitokea siku moja na nikasema haiwezi kutokea tena.Nilikuwa nimepanga nikupitie kabla ya kuelekea nyumbani.
7. **Granma:** Habari ya John? Siku hizi hanitembelei tena!
8. **Jane:** Amesafiri wiki mbili zilizopita kwenda Dubai, kisha akitoka Dubai ataelekea Brazil kabla ya kurejea nyumbani . Hatujawasiliana tangu aondoke na sijui yuko wapi kwa wakati huu.
9. **Granma:** Yaani alienda safari ya mbali bila kuniaga?

- 10. Jane:** Bibi siku hizi simuelewi tena John. Ofisi yake ndio hiyo hapo, lakini nadra sana kuzungumza naye. Ni milolongo ya wasichana tu wakingia na kutoka baada ya kuwapa pesa. Mara nyingine hutoka mapema ofisini lakini atakuwa mtu wa mwisho kufika nyumbani. Kila mara hutuamsha mimi na Baba usiku wa manane.
- 11. Granma:** Nini? Nani? John? Yule mvulana ambaye hakutaka kusikia mambo ya wasichana?
- 12. Jane:** Bibi, mjukuu wako sasa amekuwa mkurugenzi mkuu wa kampuni ya "Appetizers of the Tropics". Hali hii humbadilisha mwanamume!
- 13. Granma:** Na babako hasemi chochote?
- 14. Jane:** Pesa zinaongea Bibi! Siku hizi hawezi kumwambia chochote.
- 15. Grandma:** Pesa ndio chanzo cha maovu yote katika ulimwengu huu! Mimi nimekuwa nikimshauri kuhusu jambo hili kila mara! Ama sivyo?
- 16. Jane:** Unajua Bibi kila mmoja anajua atakavyotumia mafunzo hayo maishani. Kwa mimi kila

ninavyozidi kuimarika kibiashara ndivyo wasi wasi wa kuporomoka unavyoongezeka.
Unajua kadri unavyopanda ndivyo unavyoumia ukiporomoka.

17. Granma: Amekwenda kufanya nini katika nchi hizo?

18. Jane: Sina habari Bibi, Mungu ndie ajuae.! Mimi alinipa sababu za kweli na uongo hapa, kwamba anakutana na watu fulani,..... na wala usiniulize ni watu wa aina gani!.

19. Granma: Oh! Ni kitambo sidhani naweza kukumbuka sura yake tena!

20. ATMO: *The intercom rings again.*

21. Jane: Samahani Bibi!
(*into the intercom*)
Nini..... nini, Bibi Sika? ... eti nani ?...Bibi Mable? Sikuwa namtarajia! ... Kwanza simjui? Lakini ni sawa mwambie aingine na sitaki wageni wengine sawa.Naweza kuchelewa na ndege yangu.

22. ATMO: *She hangs up*

23. Granma: Na wewe je unaenda wapi?

24. **Jane:** Nasafiri kwenda Ujerumani, kwanza.
25. **ATMO:** *Somebody knocks at the door*
26. **Jane:** Karibu ndani!
27. **ATMO:** *Door opening and closing*
28. **Jane:** Naenda kukutana na Fo Blam anijulishe baadhi ya wafanyi biashara nchini Ujerumani. Kisha nitaelekea nchini Switzerland kwa kuhudhuria kozi fulani.
29. **Mrs Mable:** Habari Bi Jane!
30. **Jane:** Nzuri ! karibu kiti ukaee. Bibi Nisubiri kidogo tu nitakupeleka nyumbani sawa **Granma:** sawa nitasubiri
31. **Jane:** Ehhe nikusaidie na nini?
32. **Mrs Mable:** Ohhh, kwani umenisahau?
33. **Jane:** Hmmm.
(thinking about it)
Ndio, wewe niiii... tulikua darasa moja mwaka wa mwisho ...sivyo?

- 34. Mrs Mable:** (*Big smile*)
Hasa!
- 35. Jane:** Sikukujua kwani watu wengi huja hapa na ndo sababu akili yangu yote ilikuwa katika biashara ya Njugu. Pia mimi si mwepesi wa kukumbuka watu. Ehhe nikusaidieje?
- 36. Mrs Mable:** (*Hesitating and sad*)
Niliwapoteza wazazi wangu wote na kwa sababu hiyo sikuweza kumaliza masomo yangu na kupata cheti. Mtoto wangu ni mgonjwa na babake hata hamjali kabisa. Ningefurahi kama unaweza kunisaidia, niko tayari kufanya kazi yoyote.
- 37. Jane:** (*A bit dry*)
Ningependa sana kukuajiri lakini kwa wakati huu hatuajiri watu. Lakini unaweza kuacha anwani yako kwa sekretari wangu, mambo yakiwa mazuri nitakuita. Samahani lakini nilikuwa najiandaa kutoka.!
- 38. Mrs Mable:** (*imploring tearfully*)
Tafadhali Bi Jane sijakula tangu jana...!
Mtoto wangu yu taabani, tafadhali nisaidie!

- 39. ATMO:** *Sound of a drawer opening, Jane takes out a note*
- 40. Jane:** Sina pesa nyingi kwa wakati huu lakini chukua hizi faranga elfu 5 zitakusaidia. Sawa.. kila la kheri!
- 41. Mrs Mable:** Asante sana Bi Jane na Mungu akubariki. Pia usinisahu kwa kazi yoyote. Asante sana!
- 42. Jane:** Sitakusahai Bi Mable.
(*To Granma*)
Tunaweza kwenda sasa Bibi!
- 43. ATMO:** *the visitor leaves*
- 44. Granma:** (*Whispering*)
Ohhh! Jane! Umebadilika sana! Huwezi kumuonea huruma yule Mama maskini?
- 45. Jane:** Yule mwanamke maskini ni miongoni mwa kundi la wanafunzi wenzangu wa kike ambao walikuwa wakinicheka shuleni nikiuza Njugu. Walikuwa wakiniita "msichana wa Njugu".
- 46. Granma:** Na hilo lilikuathiri vipi?. Kati ya wee na yeye nani anamuhitaji mwenzake zaidi wakati

huu? Mjukuu wangu usiwe mtu wa kulipiza kisasi kwa watu waliokukosea.

- 47. ATMO:** *They leave the office, which Jane locks.*
- 48. Granma:** *(To Mrs Sika)*
Kwaheri mwanangu.
- 49. Mrs Sika:** Kwaheri Mama uwe na safari njema Bi Jane!
- 50. Jane:** Asante Bibi Sika! Nawe ubaki salama, Nitakupigia simu kesho kukujulisha mahali nitakako kuwa naishi .Bw John akirudi au akikupigia simu mpe ujumbe .
- 51. ATMO:** *Sound of the door. They get into the car.
Jane drives off.*
- NARRATOR:** Jane anaingia ndani ya gari lake na kumpeleka Bibi nyumbani , na kisha kwenda nyumbani kwake kubadilisha na kuelekea moja kwa moja hadi uwanja wa ndege.

Scene 2, AT THE AIRPORT

JANE, DAD...

- 52. ATMO:** *At the airport, luggage carriers hurry around with carts.*

- 53. Dad:** Huwa nasikia furaha kila wakati ninapokupeleka uwanja wa ndege. Wafanyi kazi wote katika idara ya mizigo wanakujua..., maafisa wa idara ya forodha wanakufahamu, wahudumu wote wa ndege pia wanakujua. Hivi karibu marubani pia watakujua!
- 54. Jane:** *(Laughing)*
Tosha Baba.... sasa unavuka mpaka!
- 55. Dad:** Nadhani hujasahau chochote.
- 56. Jane:** Hapana... nafikiri nimebeba kila kitu...
- 57. ATMO:** *In the departures hall. Passengers are chatting, waiting.*
- 58. Jane:** Sawa Baba, tukutane ukumbini baada ya mimi kukaguliwa...
- 59. Dad:** Sawa na uwe mwangalifu.
- 60. Jane:** Usiwe na shaka Baba sasa nimekuwa msichana mkubwa !

61. **ATMO:** *Music while Jane checks in her luggage. She arrives at the bar. Announcements in the background.*
62. **Stewardess:** *(PA sound)*
Abiria wote wa ndege BA 527 kuelekea mjini London tafadhali mpitie lango nambari 7 kuingie katika ndege yenu.
63. **Dad:** Umemaliza?
64. **Jane:** Sasa tunataka **juice** baridi sana !
65. **Dad:** *(To the waitress)*
Binti yangu !
(To Jane) Mpaka unatokwa na jasho!
66. **Jane:** Mizigo umepita uzani unaokubaliwa. Imenichukua muda mrefu kuwashaiwi wanibebee mizigo yote. *(To the waitress)*
Nipe **juice** baridi tafadhali.
67. **Dad:** Baridi sana tafadhali.
68. **Jane:** *(Laughs)*
Baba, Bibi amechoka, na nimemshauri asiende tena sokono. Tafadhali hakikisha anafuata maagizo yangu, sawa?

- 69. Dad:** Sawa nitamtembelea kesho kuhakikisha hajaenda.
- 70. ATMO:** *A plane lands in the distance*
- 71. Jane:** Nafikiri hiyo ni ndege yangu imetua...
- 72. Dad:** Na kuhusu John?
- 73. Jane:** Unataka niseme nini Baba, John sasa ni Mtu mkubwa, siwezi kumwambia chochote..
- 74. ATMO:** *Some very loud passengers arrive.*
- 75. Jane:** Baba, mimi na John ni mapacha. Tumepitia mengi mazuri na mabaya, taabu na raha, tangu tumboni mwa marehemu Mama . Lakini sasa inavyoonekana ni kwamba huu ufanisi umeanza kututenganisha .Kila mara najaribu kuzuia machungu yangu moyoni nisiwaudhi wewe na Bibi.
- 76. Stewardess:** *(PA sound)*
Abiria wa ndege LH 347 kuelekea Frankfurt mwelekee kwenye ndege yenu kupitia lango nambari 3.

77. Jane: Hiyo ni ndege yangu Baba ,lazima nianze kwenda. Baki salama Baba, Kwaheri. Take care of yourself!

78. Dad: Safiri salama Binti yangu nakutakia kila la kheri!

79. Jane: Asante Baba!

Outro

NARRATOR: John na Jane sasa wametimiza ndoto yao ya kuwa wanabiashara mashuhuri.Safari yao ya kufika kileleni kama wafanyi biashara mashuhuri imetimia kutokana na juhudi za kubania matumizi yao. Lakini sasa kama walivyosema wahenga,pesa ni mvunja mlima na ndicho chanzo cha maovu yote.Ufanisi huu umewatenganisha na kuanza kuishi kama mbingu na ardhi baina ya viwanja viwili vya ndege.John amepagawa na shetani pesa huku Jane naye akifunga safari kuelekea nchini Ujerumani na Switzerland

80. Closing soundtrack to be left running after the outro and brought up

NARRATOR: Jeuri na ubadhirifu wa John utamfikisha wapi?Je Jane anastahili kupitia mashaka anayopitia hivi sasa. Kwa

mengi zaidi ungana nasi kwa kipindi kijacho cha Learning By Ear ujue mengi kuhusu maisha ya mapacha hawa wawili. Pia ukipenda kusikiliza tena makala haya, au kutuma maoni usisite. Tembelea mtandao wetu wa **[dw-world.de/l b e](http://dw-world.de/lbe)**

Hadi wakati mwengine tutakapoungana nawe tena
Kwaheri!

Music to be turned up

END